KNQA/025/2021-2023	Kazi za ujenzi, ugawaji, ukarabati, ujenzi na uchoraji wa majengo na ofisi, huduma za mabomba na marekebisho madogo ya kimuundo. (WAZI KWA WOTE)

Waombaji wanaohitajika wanaweza kupakua hati ya usajili kutoka kwa tovuti ya mamlaka; www.knqa.go.ke bila malipo.

Mahitaji maalum ya ziada yatatolewa kwa mamlaka kama ilivyoorodheshwa katika 2.4

Hati kamili ya usajili inapaswa kuambatanishwa katika bahasha zilizofungwa, zilizowekwa nambari ya kitengo na maelezo ya Bidhaa na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni, Orofa ya 4, Jengo la Makao Makuu ya NACOSTI, Upper Kabete kando ya Waiyaki Way, Nairobi au kutumwa kwa:

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Kitaifa ya Uhitimu Kenya,
S.L.P 72635-00100,
Nairobi.

ili kupokelewa mnamo au kabla ya tarehe 8 Agosti, 2023 saa 11.00 asubuhi.



National feed strategy aims to boost livestock resilience and productivity

BY ERASTUS GICHOHI (KNA)

The Government needs to marshal more than Sh. 460 billion within the next 10 years to implement the National Feed Strategy that seeks to address a livestock feed deficit of 33 million metric tonnes every year.

The strategy will address the shortage through the promotion of 14 animal feed value chains which have energy-rich sources, adequate minerals, and vitamin concentrates.

This comes after it emerged that Kenya has lost 2.5 million livestock in the last two years following a prolonged drought that also led to starvation of animals for lack of quality feed.

According to Stanley Mutua, the Head of Animal Feeds and Nutrition Services at the Ministry of Agriculture, Kenya requires 55 million metric tonnes of animal feed annually but produces 40 per cent leaving a huge supply gap of 33 million metric tonnes every year.

"The current animal feed deficit stands at 33 million metric tons and the government requires to inject Sh460 billion in the next 10 years to address the shortage by implementing the National Feeds Strategy," said Dr. Mutua.

He said the Government, in collaboration with other non-state actors, will support investments in five key value chains to address the



Ng'ombe wa maziwa katika Naivasha Research Institute wakati wa maonyesho ya wakulima yaliyoandaliwa na Kenya Agricultural Research Organization hivi majuzi.

gap including pasture, sorghum, sunflower, cotton, and maize silage.

Speaking in Naivasha during the African Union-backed Resilience African Feed and Fodder Systems project, Dr. Mutua said the government has instituted technical, policy actions, and institutional interventions to support and upscale the production of feeds for livestock which

Upungufu wa chakula cha mifugo sasa ni tani 33 milioni - Stanley Mutua

millions of Kenyans depend on for a living.

The head of the animal feeds docket said the government's national feed strategy will help to address animal feeds and water shortage for livestock, feed quality, costs, and weak policies and strengthen feed data and information systems to inform better and timely interventions.

In addition, Dr. Mutua said the national government is already implementing various projects for fodder commercialization in the counties to help cushion farmers and other actors in the livestock value chain from adverse effects of climate change such as pro-

longed droughts, and other global crises such as the ongoing Russia-Ukraine war.

Dr. Christopher Wanga, the Director of Livestock Policy Research and Regulations at the Agriculture Ministry said animal feeds take up to 70 per cent of all inputs required by farmers with the high costs driving the use of low-quality feeds, leading to low productivity.

"Some 2.5 million livestock have died in the last two years as a result of drought and subsequent starvation as farmers lacked timely, cost-friendly, and quality animal feeds. This resulted in loss of livelihoods to millions of families," said Dr. Wanga.

Dr. Wanga said the livestock sector contributes 50 per cent to the total agricultural sector's Gross Domestic Product (GDP), and there's a need to undertake informed research and policy decisions to support the sector by addressing the current deficit of quality feeds.

The Director said the government is working on a livestock masterplan to build resilience, strengthen research capacity and upscale viable and innovative approaches to cushion the sector from external shocks.

The masterplan also aims at ensuring production of quality livestock products such as meat, milk, and eggs that meet the nutrition demands of the citizens.

LVBC kupata makao makuu ya kisasa Kisumu



Sehemu ya jengo la Lake Victoria Basin Commission (LVBC) mjini Kisumu.

NA CHRIS MAHANDARA (KNA)

Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) imetenga Sh355 milioni kumilisha ujenzi wa makao makuu ya Tume ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) mjini Kisumu.

Katibu Mkuu Mtendaji wa LVBC, Dk Masinde Bwire alisema, mgao huo ambao umechangiwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki utawezesha shirika hilo lililopewa jukumu la kura-tibu maendeleo endelevu na usimamizi wa Bonde la Ziwa Victoria kuhamia jengo jipya Februari 2025.

Akizungumza baada ya kukabidhi eneo la Awamu ya Pili ya mradi huo, Dk Bwire alisema mwana-kandarasi- China Jiangxi International Kenya Limited ana hadi wiki 80 kukamilisha mradi huo.

LVBC, alisema, imeshirikiana na Idara ya Serikali ya Kazi za Umma ili kuhakikisha kuwa mradi huo unakamilika kwa

wakati ndani ya bajeti iliyowekwa.

Dk Bwire alisema mwana-kandarasi huyo alipatikana kwa ushindani na kuongeza kuwa shirika limeweka mikakati ya kuhakikisha kazi inafanyika kwa viwango vilivyowekwa.

LVBC ndiyo taasisi pekee ya EAC yenye makao makuu nchini Kenya na afisi zaz pekee wa kidiplomasia nchini nje ya Nairobi.

Jengo hilo ambalo linajengwa katika mwambao na Ziwa Victoria, linatarajiwa kusaidia katika uratibu mzuri wa huduma za shirika hilo.

Naibu Mbunifu Mkuu wa Idara ya Serikali ya Utumishi wa Umma David Waititu alieleza matumaini kuwa mradi huo, ambao umechukua muda mrefu kukamilika, utatekelezwa ndani ya muda uliowekwa.

"Tuko hapa ili kuendeleza mradi huo. Ni jengo la kihistoria," alisema.



TENDER NOTICE

The Kenya Electricity Transmission Company Limited (KETRACO) is a State Corporation whose mandate is to plan, design, construct, operate, own, and maintain high voltage national electricity transmission grid and regional power interconnectors.

KETRACO invites bids from all interested and eligible bidders for the tenders described below:

S/ no	Tender Description	Tender Reference Number	Eligibility	Closing Date	Time
1.	Expressions of Interest for Consulting Services for Capacity Building Needs Assessment	KETRACO-PT-021 -2023	Open	31 st August 2023	10: 30 AM EAT
2.	Request For Proposal for Provision of Staff Pension Scheme Management Services (Umbrella Scheme)	KETRACO-PT-022 -2023	Open	22 nd August 2023	10: 30 AM EAT

KETRACO tenders run on SAP ARIBA e – procurement platform and therefore tender documents detailing the requirements may be viewed at KETRACO e – procurement portal found on the KETRACO website (www.ketraco.co.ke) starting from **Tuesday 1st August 2023**.

Tender enquiries, clarifications and/or addendums to croano@ketraco.co.ke, gngugi@ketraco.co.ke, sakuto@ketraco.co.ke, jamwayi@ketraco.co.ke and irotich@ketraco.co.ke. Complete bid documents should be electronically submitted through SAP ARIBA platform on or before the closing dates.

Bids will be opened electronically promptly thereafter in the presence of the Tenderers or their representatives who choose to attend in **KETRACO Supply Chain Management Offices at KAWI House, South C, Nairobi**

SENIOR MANAGER, SUPPLY CHAIN
FOR: MANAGING DIRECTOR



MWALIKO KUSHIRIKI TENDA

Kenya Power inaalika wauzaji bidhaa kutoa huduma zifuatazo:-

NAMBARI YA TENDA	MAELEZO YA HUDUMA	TAREHE YA KUWANZA KWA TENDA	MKUTANO WA AWALI	TAREHE YA MWISHO
KP1/9A.2/OT/003/RA/23-24	Utoaji wa Huduma za Sheria na Uhasibu wa Usimamizi	Jumatano 02.08.2023	Jumatano 09.08.2023 saa 4.30 asubuhi. (Stima Plaza Auditorium)	Jumatano 16.08.2023 saa 5.00 asubuhi.

Stakabadhi za tenda zenye maelezo kamili kuhusu tenda iliyotajwa hapo juu zinaweza kupatikana katika wavuti wa Kenya Power (www.kplc.co.ke) kuanzia tarehe iliyotajwa juu.

MENEJAMKUU
UNUNUZI

www.kplc.co.ke

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy

www.kplc.co.ke | [Kenya Power](https://www.facebook.com/KenyaPower) | [Kenya Power](https://www.instagram.com/KenyaPower) | [Kenya Power](https://www.youtube.com/KenyaPower) | 0703-070 707, 0733-170 170

Mkuu wa Utumishi wa Umma akerwa na kutotumiwa kwa rasilimali nyingi Marsabit

NA SEBASTIAN MIRITI
(KNA)

Mkuu wa Wafanyakazi na Mkuu wa Utumishi wa Umma Bw Felix Koskei amekashifu kutotumiwa kwa rasilimali nyingi katika Kaunti ya Marsabit ambazo zinaweza kuzalisha mali na kubadilisha maisha ya jamii za eneo hilo.

Wakati huo huo, Koskei amewahakikishia wakazi wa kaunti hiyo kuwa serikali itaendelea kuanzisha miradi ya maendeleo inayolenga ustawi wao na kuzitaka jamii za eneo hilo kuishi kwa amani.

Mkuu wa Utumishi wa Umma, ambaye alizun-



Mkuu wa Wafanyakazi na Utumishi wa Umma Felix Koskei akiwa ktika kituo cha kibiashara cha Kargi, kaunti ya Marsabit alipotembelea eneo hilo kukagua miradi ya maendeleo katika kaunti ndogo ya Loiyangalani.

gumza huko Kari alipofanya ziara ya siku mbili katika kaunti ndogo ya Loiyangalani eneo bunge la Laisamis kutathmini mahitaji ya huduma kwa wenyeji, alidokeza kuwa eneo hilo lina rasilimali nyingi ambazo zikitumiwa, zinaweza kutengeneza ajira na kuzalisha mali.

Akiitikia mwito wa wakazi na viongozi ambao ni pamoja na Mbunge wa eneo hilo Bw Joseph Elkton na Naibu gavana Bw Solomon Gobo, Koskei alitaja kuwepo kwa uwezo mkubwa katika utalii, madini, uvuvi, ufugaji na biashara ya mifugo ambayo ikitumiwa inaweza kubadilisha maisha ya watu.

Alibainisha kuwa hili litafikiwa iwapo kutakuwa na mazingira wezeshi kwa uwekezaji na kuwataka wazee na viongozi kujenga amani

na uaminifu miongoni mwa jamii.

Hivyo basi, Koskei alitoa changamoto kwa uongozi wa eneo hilo kuunda mipango ya maendeleo ambayo inaweza kufanikisha matumizi ya rasilimali zilizopo kwa ajili ya kuboresha hali ya maisha ya wakazi.

Hilo litawezekana tu, akaongeza, ikiwa jamii zitakumbatia elimu na akaelekeza Kamishna wa Kaunti Bw Norbert Komora kuhakikisha kwamba watoto wote walio na umri wa kwenda shule wameandikishwa shuleni bila kujali jinsia.

"Ningependa Kamishna wa Kaunti ahakikishe kuwa idara husika pamoja na wazazi na walezi wanatekeleza majukumu yao inavyotarajiwa kwa sababu watoto wote wanapaswa kupata elimu bila ubaguzi kama haki ya kimsingi na ya kisheria," akaagiza.

Akikiri kwamba mengi yanahitajika kufanywa katika takriban sekta zote, Koskei alisema serikali itazingatia ujenzi wa bweni la shule katika Kata ya Kargi huku Barabara ya Hula-Hula Loiyangalani ikiboreshwa hadi kiwango cha lami.

Serikali yazindua jukwaa la iTATU ili kukuza ushirikiano wa wasomi

NA ALI SHEIKH MOHAMMED
(KNA)

Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda kupitia mradi wa Viwanda na Ujasiriamali wa Kenya (KIEP), imezindua jukwaa la wasomi linalolenga zaidi wanafunzi linaloitwa iTATU (waza, vumbua na utekeleze).

Jukwaa limeundwa ili kuwezesha vyuo na vyuo vikuu na wanafunzi wao kushirikiana na kampuni binafsi kwa utengenezaji wa bidhaa mahususi.

Wizara ya Uwekezaji imeshirikiana na Shule ya Usimamizi ya Maastricht kusaidia wabunifu kupata ushauri wa mtandao ili kuwawezesha kuwa wajasiriamali wapa na ulinzi wa mali miliki kwa kushirikiana kwa faida.

Katibu wa Wizara ya Viwanda, Juma Mukhwana, alisema Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Kiu-fundi vina wajibu wa kufanya utafiti huku akibainisha kuwa tafiti nyingi hazifanyiki kibiashara.

Waziri Mkuu alisema hayo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu wa Utawala wa Idara ya Kitaifa ya Viwanda Karanja Njora wakati wa uzinduzi wa jukwaa la iTATU jijini Nairobi.

Dkt Mukhwana alisema kuna haja ya kubuni mtindo ambao unaweza kujiendeleza wa jukwaa



Katibu wa Usimamizi katika Idara ya Viwanda Bw Karanja Njora (tatu kulia) na mwakilishi wa Benki ya Dunia Bw Sameer Goyal wakati wa uzinduzi wa jukwaa la iTATU katika Nairobi Garage Promenade, Westlands mnamo Jumanne iliyopita.

la wasomi. "Hii itafungua miundo ya ubunifu ambapo viwanda vinaweza kuchapisha changamoto zao na kuwaalika wanafunzi wabunifu, na pia kuwaweka kwenye njia ya kuunda njia endevu za ujasiriamali," Dkt Mukhwana alisema.

Wakati huo huo alibainisha kuwa Kenya inataka kuwa na ushindani wa kimataifa kupitia ajenda ya mabadiliko ya kiuchumi kutoka chini kwenda juu kwa kuunda kundi endevu la biashara ndogo ndogo na za kati kulingana na Mpango wa Nne wa


Muda wa Kati 2023-2027.

Waziri alisisitiza zaidi ushirikiano kati ya wasomi na sekta hiyo akisema itaendesha ubunifu, maendeleo ya bidhaa mpya na ushindani wa viwanda.


"Ulimwengu uko katika hatua ya mabadiliko makubwa katika jinsi uchumi unavyopangwa na kuendeshwa na msukumo wa uendelevu kupitia kupitisha utengenezaji unaojulikana kama Kijani na Mapinduzi ya 4 ya Viwanda (sekta 4.0) ambao unakuza matumizi robotiki, uchapishaji wa 3D na uhandisi wa maumbile. Mwakilishi

wa Benki ya Dunia Sameer Goyal alisema Benki ya Dunia ilianza mradi huo mnamo 2019 lakini ilipunguzwa kasi na janga la Covid-19. "Nchi bado inapata nafuu kutokana na janga hili ambalo lililemaza mpango huu ambao tulianza zamani lakini sasa unashika kasi," Bw Goyal alisema.

Alisema wanafunzi wana mawazo mazuri yanayoweza kubadilika na kuwa teknolojia ambayo yatawafanya kuwa wabunifu na wajasiriamali katika ulimwengu huu wa ushindani wa biashara.



KENYA COPYRIGHT BOARD




TENDER NOTICE


This is to notify the public that a tender for sale of motor vehicle make Land Rover Defender has been uploaded onto the Kenya Copyright Board website, and may be downloaded from www.copyright.go.ke.

Tenders will be opened in the presence of candidates or their representatives who choose to attend, at Kenya Copyright Board, Boardroom, NHIF Building, 5th Floor Ragati Road Nairobi, at **11.00 am on WEDNESDAY 9th August 2023**


Note: The vehicle may be viewed at NHIF building after notifying the Transport Officer, Kenya Copyright Board between 9.00 am and 3.00pm during official work days.


The Executive Director





MINISTRY OF EDUCATION





KNEC is ISO 9001:2015 Certified

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

NOTISI YA TENDA

Kenya National Examinations Council (KNEC) ni shirika la kiserikali lililoanzishwa mnamo 1980 chini ya Kifungu cha Sheria ya Bunge, Sura ya 225A ya (1980). Sheria hiyo ilitatiliwa mnamo 2012 na mahali pake kuchukuliwa na Sheria ya Baraza Nambari 29, 2012. Baraza limepewa jukumu la kusimamia mitihani katika ngazi ya kitaifa katika taasisi za elimu msingi na juu na kuwatuza watahiniwa vyeti.


1.0 Kenya National Examinations Council (KNEC) sasa inaika maombi ya kushiriki tenda kutoka kwa taasisi mbalimbali kushiriki tenda ifuatayo:

S/No.	NAMBARI YA TENDA	JINA LA TENDA
1.1	KNEC/ONT/2023-2024/01	Utoaji wa Huduma za Bima ya Afya kwa Afisa Mkuu Mtendaji, Wanchama wa Bodi na Wafanyakazi (ile ya kutibiwa na kuenda nyumbani na pia ya kulazwa)

2.0 Washiriki wanaweza kupata stakabadhi za tend kutoka kwa wavuti zifuatazo: www.knec.ac.ke or www.supplier.treasury.go.ke au www.tender.go.ke

3.0 Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni **Agosti 11, 2023 saa 4.00 asubuhi**. Nafasi ya kutuma maombi iko wazi kwa kila mtu. Maombi yatakatyotumwa kuchelewa yatakataliwa.

AFISA MKUU MTENDAJI





NAFASI ZA KAZI

Jumba la Kimataifa la Mikutano la Kenyatta (KICC) limeanzishwa chini ya Sheria ya Utalii, Na. 28 ya 2011 (Sheria hiyo). Jukumu la KICC ni kukuza biashara ya mikutano, makongamano na maonyesho. Hii inahusisha:-

1. Kutayarisha na kuandaa mikutano na kutoa motisha kwa makongamano na maonyesho katika Kituo cha Mikutano;
2. Kuandaa na kutekeleza mikutano ya kitaifa, mkakati wa makongamano na maonyesho kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii baada ya kushauriana na wadau husika;
3. Uuzaji wa Kituo cha Mikutano, kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii; na;
4. Kutekeleza majukumu mengine yoyote ambayo ni ya ziada kwa lengo na madhumuni ambayo Kituo cha Mikutano kimeanzishwa.

KICC iko katika harakati za kuajiri watu wanaofaa na inakaribisha maombi ya nyadhifa zifuatazo:

Na	Marejeleo	Nafasi ya Kazi	Daraja	Idadi
1	KICC/CEO/2023	Afisa Mkuu Mtendaji	KICC 1	1
2	KICC/CS/2023	Katibu wa Shirika	KICC 2	1

Afisa Mkuu Mtendaji- Daraja la Kazi, KICC 1

a. Kusudi la Kazi

Afisa Mtendaji Mkuu (CEO) atakuwa mkuu mtendaji wa Kituo na anawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa usimamizi na uratibu wa shughuli za kila siku katika Bodi.

b. Maelezo ya Kazi

Wajibu na majukumu katika ngazi hii yanajumuisha;

- (i) Katibu wa Bodi
- (ii) Msemaji Mkuu wa Shirika
- (iii) Kuratibu shughuli na shughuli za usimamizi za Shirika;
- (iv) Kuandaa sera na programu za Shirika;
- (v) Kusimamia fedha na mali na rasilimali nyingine za Shirika;
- (vi) Kusimamia na kuendeleza wafanyakazi katika Shirika;
- (vii) Kuandaa mipango ya uendeshaji na programu kwa ajili ya kufikia malengo ya Shirika;
- (viii) Kuendeleza muundo wa usimamizi wa ndani wa kiuchumi, ufanisi na wa gharama nafuu;
- (ix) Kusimamia utekelezaji na mapitio ya Mpango Mkakati, mpango wa biashara na mpango wa mwaka wa Shirika;
- (x) Kuhakikisha utekelezaji na utimilifu wa sera na malengo yaliyokubaliwa; malengo ya utendaji na viwango vya huduma vya Shirika.
- (xi) Kutoa ushauri kama inavyohitajika katika masuala yote ndani ya mamlaka ya Kituo;
- (xii) Kutekeleza wajibu mwingine wowote muhimu kama ilivyoainishwa katika Sheria husika.
- (xiii) Kufanya kazi nyingine yoyote ambayo inaweza kuamuliwa na bodi ya kituo cha mikutano

c. Vigezo vya kazi

Kwa uteuzi wa daraja hili, afisa lazima:-

- (i) Awe na uzoefu usiopungua miaka kumi (10) katika ngazi ya uongozi wa juu katika utalii, ukarimu au sekta inayohusiana;
- (ii) Awe na Shahada ya Kwanza kutoka katika taasisi inayotambulika;
- (iii) Awe na shahada ya uzamili katika usimamizi wa biashara ya masoko au taaluma inayohusiana
- (iv) Awe mwanachama wa chombo cha kitaaluma;
- (v) Awe na cheti cha Kozi ya Uongozi kisichopungua wiki nne (4) kutoka kwa taasisi inayotambulika;
- (vi) Awe na ujuzi katika matumizi ya kompyuta;
- (vii) Onyesha umahiri wa kitaaluma na uwezo wa usimamizi kama unavyoonyeshwa katika utendaji na matokeo ya kazi.

Katibu wa Shirika - Daraja la Kazi, KICC 2

a. Kusudi la Kazi

Kukipa Kituo ushauri wa kisheria, kushughulikia kesi mahakamani na kuhakikisha utiifu wa mahitaji ya kisheria na kisheria ndani ya Baraza.

b. Maelezo ya Kazi

Wajibu na majukumu katika ngazi hii yatajumuisha:

- (i) Kusimamia majukumu ya Kurugenzi ya utawala k.m ripoti za utendaji kazi, masuala ya wafanya kazi na kuendeleza na kuboresha mifumo ya Kurugenzi, taratibu na udhibiti wa ndani.
- (ii) Kutoa mwongozo kwa bodi kuhusu kazi na wajibu wao na masuala ya Utawala.
- (iii) Kuisaidia Bodi katika kutekeleza utangulizi na mafunzo ya Bodi, kusasisha hati za bodi na kamati, kuandaa mipango kazi ya Bodi, tathmini ya Bodi, Ukaguzi wa Utawala Bora, utekelezaji wa kanuni za maadili na maadili.
- (iv) Maandalizi na mapitio ya mkataba wa bodi ya Mashirika na vyombo vya bodi.
- (v) Kuhakikisha utayarishaji na usambazaji kwa wakati karatasi na muhtasari wa Bodi na Kamati.
- (vi) Awe mtunzaji wa mhuri wa Shirika na kuwajibika kwa Bodi kwa matumizi yake.
- (vii) Kuhakikisha wajumbe wa Bodi wanafahamu sheria zinazohusu shirika.
- (viii) Kuwezesha mawasiliano yenye ufanisi kati ya Shirika, na wanahisa/wadau.
- (ix) Hakikisha kwamba marejesho ya mwaka yanawasilishwa kwa mamlaka husika mara moja.
- (x) Kuwezesha shughuli za bodi ndani na nje ya nchi.

- (xi) Kudumisha na kusasisha rejista ya mgongano wa maslahi.
- (xii) Kuhakikisha uhifadhi salama wa vyombo vya kisheria vya Shirika, nyaraka za Kisheria, hati fungani za utendaji kazi, dhamana na mali/Mali nyingine zote za Shirika.
- (xiii) Kupitia na kushauri Usimamizi na Bodi kuhusu athari za kisheria za sera za ndani na taratibu.
- (xiv) Kuwakilisha Bodi katika shughuli za ushirika na utatuzi wa migogoro.
- (xv) Kusimamia Mashirika ya kukodisha na Madai.
- (xvi) Kufanya taratibu za Kisheria za tathmini ya hatari kwa lengo la kubaini hatari zinazoweza kutokea na kutoa hatua zinazofaa za kupunguza.
- (xvii) Hakikisha kuwa Mali ya Uvumbuzi ya shirika, (IP), inalindwa na kulindwa.
- (xviii) Kutoa jukumu la usimamizi kwa huduma za Sheria na Udhibiti kupitia ukaguzi wa mara kwa mara na tathmini ya kazi za idara, mapitio ya mikataba yote mikuu, kesi za mahakama masuala mengine yoyote yanayohusiana.
- (xix) Kuwasiliana na Idara ya Rasilimali Watu katika kufanya tathmini ya utendaji kazi na kuhakikisha mapungufu ya uwezo na mafunzo yanatatuliwa.

c. Vigezo vya kazi

Kwa uteuzi wa daraja hili, afisa lazima awe na:-

- (i) Shahada ya Kwanza ya Sheria.
- (ii) Shahada ya Uzamili ya Sheria.
- (iii) Mwanachama wa Chama cha Wanasheria wa Kenya (LSK) aliye na sifa nzuri na aliye na cheti cha sasa cha utendakazi.
- (iv) Mwanachama wa Taasisi ya Makatibu wa Umma Walioidhinishwa wa Kenya (IPSK) aliye na hadhi nzuri.
- (v) Mthibitishaji wa Umma na Kamishna wa Viapo.
- (vi) Uzoefu wa kazi husika usiopungua miaka 10, 5 kati yake uwe katika nafasi ya usimamizi.
- (vii) Kufahamu sheria zote zinazohusu shirika, kanuni za utawala zinazohusika kujumuisha Sheria ya Utalii ya 2011.
- (viii) Ujuzi mzuri juu ya taratibu na kanuni za Bodi, Utawala Bora na masuala mengine yanayohusiana nayo.
- (ix) Awe amejiozoeza kama wakili kwa muda usiopungua miaka 7.
- (x) Cheti cha Uongozi kinachochukua muda usiopungua wiki nne (4).
- (xi) Ufahamu katika matumizi ya Kompyuta.

Maombi:

Maombi lazima yazingatie Sura ya 6 ya katiba na kupata hati za kibali kutoka kwa:-

- IDARA YA UPELELEZI WA JINA! (CHETI CHA MWENENDO MZURI)
- UZINGATIAJI WA USHURU WA MAMLAKA YA KUKUSANYA USHURU KENYA (KRA)
- BODI YA MIKOPO YA JUU (HELB)
- TUME YA MAADILI NA KUPAMBANA NA UFISADI (EACC)
- OFISI YA MAREJELEO YA MIKOPO (CRB)

Watu wenye nia na waliohitimu wanaombwa kuwasilisha maombi yao ambayo yatajumuisha:-

1. Taarifa ya ukurasa mmoja kuhusu jinsi unavyokidhi mahitaji ya nafasi hiyo
2. Wasifukazi
3. Onyesha mshahara wa sasa
4. Vyeti vya kitaaluma na ushuhuda
5. Wadhamini watatu kitaaluma

Masharti ya Uajiri

Wajibu na majukumu katika ngazi hii yanajumuisha;

Uteuzi wa mgombea aliyefaulu utakuwa kama ifuatavyo:-

i. Daraja la 1 la kazi litateuliwa kwa mkataba wa miaka mitatu (3) unaoweza kurejeshwa mara moja kulingana na utendakazi.

ii. Daraja la Kazi KICC 2 litateuliwa kwa kandarasi ya miaka mitano (5) inayoweza kurejeshwa kulingana na utendakazi.

Maombi yanapaswa kutumwa chini ya kifuniko cha siri na bahasha iliyoandikwa kulingana na Rejeleo lako la ombi.

**"Mint: KICC/.....2023....." isipite
Tarehe 23 Agosti saa 5.00 jioni kwa:-**

**Afisa Mkuu Mtendaji
Jumba la Kitaifa la Mikutano la Kenyatta
P O Box 30746 - 00100
NAIROBI**

Tutawasiliana tu na wagombea watakaorodheshwa, watu wenye mahitaji maalum ambayo yanakidhi mahitaji wanahimizwa kutuma maombi.

**AFISA MKUU MTENDAJI
JUMBA LA KITAIFA LA MIKUTANO LA KENYATTA**





Kenya Tsetse and Trypanosomiasis Eradication Council (KENTTEC)



Baraza la Kumaliza Virus vya Tripanosomiasis Kenya (KENTTEC) lilianzishwa kupitia Notisi ya kisheria Na. 77 ya tarehe 27 Julai 2012 chini ya Sheria ya Mashirika ya Serikali Sura ya 446. Lina mamlaka ya kuwa wakala wa Serikali kuhusu mikakati, uhamasishaji wa rasilimali, uhusiano na uratibu wa tsetse na Utokomezaji wa Trypanosomiasis nchini Kenya.

KENTTEC inakaribisha hati za zabuni zilizofungwa kutoka kwa kampuni zinazostahiki kutoa zabuni kwa aina zifuatazo za Bidhaa, Huduma na Huduma za Ushauri inapohitajika katika kipindi kinachoshia tarehe 30 Juni 2024.

KITENGO A: USAMBAZAJI BIDHAHA				
S.NO	NAMBARI YA MAREJELEO YA ZABUNI	MAELEZO YA ZABUNI	UHITIMU	DHAMANA
1.	KENTTEC/1/2023-2024	Usambazaji wa Deltamethrin 5% EC	Imehifadhiwa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu	Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
2.	KENTTEC/2/2023-2024	Usambazaji wa Alphacypermethrin 10% EC	Wazi	Dhamana ya Ksh.100, 000 kutoa kwa benki inayotambulika au Kampuni ya Bima inayokubalika (Makampuni Yasiyo ya AGPO). Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
3.	KENTTEC/3/2023-2024	Usambazaji wa Flumethrin 1% EC	Imehifadhiwa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu	Zabuni zilizotengewa Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
4.	KENTTEC/4/2023-2024	Usambazaji wa Phenols/Harufu za Tsetse	Imehifadhiwa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu	Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
5.	KENTTEC/5/2023-2024	Usambazaji wa Deltamethrin-Viua wadudu Malengo/Skrini na Malengo Madogo	Wazi	Dhamana ya Ksh.500, 000 kutoa kwa benki inayotambulika au Kampuni ya Bima inayokubalika (Makampuni Yasiyo ya AGPO). Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
6.	KENTTEC/6/2023-2024	Usambazaji wa Fences Protective Fences (LPF)-(Deltamethrin Treated Zero Grazing net)	Wazi	Dhamana ya Ksh.100, 000 kutoa kwa benki inayotambulika au Kampuni ya Bima inayokubalika (Makampuni Yasiyo ya AGPO). Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
7.	KENTTEC/7/2023-2024	Ugavi wa vitendanishi vya Maabara na kemikali za shambani kwa uchambuzi wa sampuli za Trypanosomiasis ya Kiafrika (AAT) na Human African Trypanosomiasis (HAT)	Imehifadhiwa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu	Zabuni zilizotengewa Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
8.	KENTTEC/8/2023-2024	Ugavi wa kompyuta za Ofisi, laptopu, iPads, EDMS, Bodi ya Kielektroniki, maunzi ya Mkutano	Imehifadhiwa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu	Zabuni zilizotengewa Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
KITENGO B: UTOAJI HUDUMA				
9.	KENTTEC/9/2023-2024	Utoaji wa huduma za bima ya wafanyakazi	Wazi	Dhamana ya Ksh.100, 000 kutoa kwa benki inayotambulika au Kampuni ya Bima inayokubalika (Makampuni Yasiyo ya AGPO). Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
10.	KENTTEC/10/2023-2024	Uchapishaji wa mpango mkakati wa KENTTEC 2023/2024-2027/2028	Wazi	Dhamana ya Ksh.20, 000 kutoka kwa benki inayotambulika au Kampuni ya Bima inayokubalika (Makampuni Yasiyo ya AGPO). Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.
KIWANGO C: HUDUMA ZA USHAURI				
11.	KENTTEC/11/2023-2024	Ushauri wa Uwekaji wa Utunzaji wa Malengo/Skrini ya Kiuadudu cha Deltamethrin katika maeneo yaliyoshambuliwa na Deltamethrin	Wazi	Dhamana ya Ksh. 200, 000 kutoa kwa benki inayotambulika au Kampuni ya Bima inayokubalika (Makampuni Yasiyo ya AGPO). Kampuni za AGPO kutoa Fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni, iliyojazwa, kutiwa muhuri na kusainiwa.

B: USAJILI/ ZABUNI YA WAKANDARASI, WASAMBAZAJI NA WATOA HUDUMA

i. Bidhaa			
S/No.	Nambari ya Marejeleo ya Kitengo	Maelezo ya Bidhaa	Uhimitu
1.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/001	Usambazaji wa vifaa vya Ofisi	Vijana, Wanawake, PWD
2.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/002	Usambazaji wa Vifaa vya Ofisi na Samani	Vijana, Wanawake, Wakemavu
3.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/003	Usambazaji wa Vifaa vya Kompyuta, Programu, Printa na Vifaa	Vijana, Wanawake, PWD
4.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/004	Usambazaji wa Matairi na Mirija	Wazi
5.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/005	Usambazaji wa Vitu na Viunga vya Umeme	Vijana, Wanawake, PWD
6.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/006	Usambazaji wa kemikali za Maabara, kemikali za shambani na vitendanishi	Wazi
7.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/007	Usambazaji wa Sare za Wafanyakazi (pamoja na Ada za CMT), Mazulia, Mapazia, Neti, Viatu na Mavazi mengine ya kinga.	Vijana, Wanawake, Wakemavu
8.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/008	Usambazaji wa Simu, rununu, Kadi za Kupiga Zilizolipiwa Mapema na Kadi za Mkwazu.	Vijana, Wanawake, PWD
9.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/009	Utoaji wa Vifaa vya Utangazaji, Jezi na Kofia zenye Chapa, Mabango, Stendi za Maonyesho na Huduma zinazohusiana.	Vijana, Wanawake, PWD
10.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/010	Usambazaji wa Vipuri vya Magari, betri na Vifaa	Wazi
11.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/011	Usambazaji wa Dawa, Sera na Chanjo	Wazi
12.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/012	Usambazaji wa kemikali za Kudhibiti Wadudu, ufukuzaji na huduma zingine zinazohusiana	Wazi
13.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/013	Usambazaji wa vifaa vya Daktari wa Mifugo na Maabara na vifaa vinavyohusiana	Wazi
14.	KENTTEC/PreQuals/Goods/2023/2024-2025/014	Ugavi, utoaji na matengenezo ya vifaa vya kuzima moto	Wazi
ii. Huduma			
15.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/015	Ukarabati na Utunzaji wa Magari. Wafanyakazi/ Garage Zilizoidhinishwa na CMTE	Wazi
16.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/016	Ukarabati wa Vifaa vya Ofisi, Vifaa vya Intaneti, Kompyuta, Simu, Fotokopi, Mashine za Faksi, utoaji wa huduma za intaneti na mashine nyingine za kifiofi.	Vijana, Wanawake, PWD
17.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/017	Matengenezo Madogo, Mabomba na Matengenezo ya Umeme	Wazi
18.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/018	Utoaji wa Huduma za Uchapishaji	Vijana, Wanawake, PWD
19.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/019	Zabuni ya makampuni kwa upigaji picha, videografia, sauti na kuona, huduma za uhariri wa uzalishaji (ikiwa ni pamoja na kubuni na DTP) na huduma jumuisi za mawasiliano ya kidijitali.	Vijana, Wanawake, PWD
20.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/020	Zabuni ya ukodishaji magari na huduma za usafiri.	Wazi
21.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/021	Zabuni ya makampuni kwa usambazaji wa maji ya chupa na vinywaji visivyo na pombe.	Vijana, Wanawake, PWD
22.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/022	Wakala wa Usafiri na huduma zinazohusiana na Kampuni Zilizojaliwa na IATA	Wazi
23.	KENTTEC/PreQuals/Services/2023/2024-2025/023	Utoaji wa huduma za bima, GPA, gari, maisha ya kikundi, n.k.	Wazi

Hati za kina za Zabuni zinaweza kupatikana kutoka Ofisi ya Manunuzi ya KENTTEC, baada ya malipo ya ada isiyoweza kurejeshwa ya **KShs.1,000.00** kwa kila kikundi kinacholipwa kwa Afisa Mkuu Mtendaji wa Halmashauri ya Kutokomeza Trypanosomiasis Kenya (KENTTEC), taslimu, Hundi au Agizo la Pesa katika ofisi ya fedha ya Halmashauri.

Hati hizo pia zinaweza kupakuliwa kutoka Tovuti ya Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma (PIIP) www.tenders.go.ke AU Tovuti ya KENTTEC www.kenttec.go.ke bila gharama yoyote. Tunawahimiza Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu kuwasilisha nyaraka za zabuni ili kuzingatiwa kulingana na ahadi za serikali chini ya Upatikanaji wa Fursa za Ununuzi za Serikali (AGPO).

Hati za zabuni iliyokamilishwa katika bahasha iliyofungwa iliyo na nambari za kumbukumbu iliyoonyeshwa kwenye jedwali hapo juu inapaswa kutimwa kwa:-

Afisa Mkuu Mtendaji
Baraza la Kutokomeza Ugonjwa wa Trypanosomiasis,
P.O. Box 66290-00800, Westlands.
AU

Imewekwa kwenye Sanduku la Zabuni katika Ofisi ya Usimamizi wa Mfumo wa Usambazaji, KENTTEC, iliyoko katika Jengo la Kituo cha Biashara cha Crescent ghorofa ya 3-Parklands mkabala na Hospitali ya MP-Shah karibu na Kituo cha Petroli cha Shell kando ya Barabara ya Parklands mnamo au kabla ya **Jumane, 16 Agosti, 2023 saa 10.00 asubuhi (Wakati wa Afrika Mashariki).**

Ufunguzi wa zabuni utafanywa mara moja mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakoamua kuhudhuria ufunguzi kwenye Chumba cha Mikutano cha Baraza.

KALRO yatengeneza mbinu jumuishi katika hatua ya kudhibiti viwavi jeshi

NA WANGARI NDIRANGU (KNA)

Wanasayansi kutoka Shirika la Utafiti wa Kilimo na Mifugo la Kenya (KALRO) wameunda Mfumo wa Kudhibiti Wadudu (IPM) ili kudhibiti viwavi jeshi nchini.

Mdudu huyo analeta changamoto kubwa kwa uchumi, mazingira na utoshelevu wa chakula nchini kwa kusababisha uharibifu wa mazao, hasara na hivyo kuongeza kutegemea bidhaa kutoka nje ili kupunguza mahitaji ya ndani.

Hata hivyo, kutokana na hatua za Serikali, wakulima wamepeleka mafunzo na mashirika husika ya kilimo kama KALRO kuhusu mbinu za hivi za kudhibiti kuenea kwa viwavi jeshi.

Watafiti kutoka KALRO wanasema kupitia hatua mbalimbali chini ya IPM, wakulima wanaweza kupata taarifa kutoka kwa data za ufuatiliaji kuhusu mienendo ya uvamizi baada ya kupata mafunzo.

Wakiongozwa na Dk. Muuo Kasina, mtaalamu wa wadudu kutoka KALRO, watafiti wanasema, dhana ya IPM ni mbinu ya jumla inayotegemea mchanganyiko wa mikakati mbalimbali ya kudhibiti wadudu, ikiwa ni pamoja na mbinu za kibayolojia, kitamaduni, kimwili na kemikali na ni endelevu zaidi na inatunza mazingira ikil-



Catherine Mutua, mkulima wa mahindi kutoka wadi ya Masii kaunti ndogo ya Mwala ambaye alinufaika na mafunzo kutoka KALRO aonyesha mahindi yake yaliyoharibiwa na viwavi jeshi

Mahindi yaliyoharibiwa na viwavi jeshi

inganishwa na kutegemea dawa za kemikali pekee.

Dkt Kasina, aliambia KNA kuwa mdudu aina ya viwavi amekuwa tishio nchini

“Mpango huu ulianza na ukaguzi, kutunza mimea na kutumia mbinu za bayolojia-Kasina

tangu 2017 wakati uvamizi mkubwa wa kwanza ulipori-potiwa katika mashamba ya mahindi.

“Tishio la uvamizi wa viwavi jeshi limesababisha wakulima kulima mahindi yenye kemikali nyingi ili kuepusha mashambulizi kwani bila kuyatibu kunaweza kusababisha kuharibika kwa mazao kwa asilimia 100,” mwanasayansi

wa KALRO alise na.

Kasina alise na ili kukabiliana na changamoto ya utoshelevu wa chakula inayoletwa na mdudu huyo, wadau wa kilimo mwaka 2019, kupitia ushirikiano na Serikali ya Korea Kusini katika mpango uliopewa jina la KAFACI, kwa kushirikiana na Wanasayansi kutoka nchi 14 za Afrika, walianza mpango wa IPM ili kudhibiti tishio la wadudu hao.

“IPM inajumuisha ujuzi tofauti wa utunzaji wa mazao, kanuni bora za afya, na lishe kwa mmea na pia inazingatia ripoti za ufuatiliaji juu ya mwenendo wa uvamizi kupitia uchunguzi na ufuatiliaji wa kuenea kwa wadudu ili kutumia hatua za udhibiti,” alisema.

Alieleza kuwa mpango wa miaka mitano na utafiti ulioanzia 2020 hadi Desemba 2022 ulijaribiwa huko Machakos ambapo jaribio la IPM lilipata matokeo ya kuvutia.

“Mpango ulianza kwa utunzaji wa mazao, ufuatiliaji, na kuongezeka kwa udhibiti wa kibayolojia. Ingawa baadhi ya bidhaa za udhibiti wa kibayolojia dhidi ya wadudu hao zinaweza kusababisha magonjwa kwa wadudu, haina madhara kwa binadamu inapotumiwa mapema vya kutosha wakati kuna uwezekano mdogo wa kushambuliwa na wadudu,” alisema.

KWA UFUPI

Serikali kuinua kilimo biashara ili kukabiliana na ukosefu wa ajira

Serikali itaendelea kutekeleza sera na kanuni za kuwahimiza vijana kujiingiza katika kilimo biashara kama ajira rasmi mbadala. Hii ni kupitia kuanzishwa kwa ushirikiano wa kibinafsi na wama ambapo vijana wanahamasishwa kuchukua kilimo ambacho kina uwezo mkubwa wa kuunda ajira na kuchochea mageuzi ya kiuchumi ya nchi. Waziri la Vyama vya Ushirika na Maendeleo ya Biashara Ndogo na za Kati (MSMEs) Simon Chelugui alibainisha kuwa kutokana na wastani wa vijana milioni moja wa Kenya kujiunga na soko la ajira kila mwaka na uhaba wa nafasi za kazi, kilimo cha kisasa ndicho fursa itakayofuata.

Kutokana na kupanda kwa bei za vyakula, Bw Chelugui alitoa changamoto kwa vijana kujitosa katika sekta hiyo na kusaidia ujumuishaji wa mbinu za kisasa na endelevu zinazolenga kupunguza gharama za uzalishaji. “Vijana wengi ni wajuzi wa teknolojia. Ni wito kwao kutumia ujuzi wa kutatua changamoto katika sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji na kuleta mapinduzi katika mfumo wa chakula duniani,” alisema.

Waziri alihimiza vya vya kiufundi, na vya vya kuanzisha kilimo biashara na vituo vya mafunzo ili kutoa jukwaa kwa wajasiriamali vijana kupata ujuzi wa kiufundi. “Ili kuhakikisha MSME zinazoongozwa na vijana hazichai nyuma katika mageuzi ya kiuchumi kutoka chini kwenda juu, kuna haja ya kukuza mazingira ya uvumbuzi kwa kuanzisha vituo vya utafiti na vitovu vya uvumbuzi vilivyowekwa kwa wajasiriamali vijana. Mkakati wa ujuzi wa sekta nzima unapaswa kuhakikisha uwiano wa msaada wa kiufundi na kujenga uwezo,” waziri alibainisha.

Akiashiria kuwa serikali imeanzisha mipango mbalimbali inayoweka mazingira wezeshi kwa vijana katika biashara ya kilimo, Bw Chelugui alisema mfumo wa elimu nchini Kenya unapaswa kuwahimiza vijana kufanya kilimo. “Tunapaswa kuacha kuwafundisha vijana wetu nadharia na badala yake tujikite katika vitendo na tafti ambazo zinaweza kutekelezwa kika-milifu na kwa urahisi,” waziri alisema.

Jane Ngugi na Dennis Rasto

Mavuno bora ya ngano ya magunia 1.2m yatarajiwa

Wakulima wa ngano nchini wamepata mavuno mengi sana na serikali inatarajia zaidi ya magunia milioni 1.2 kutoka kote nchini. Katibu wa Idara ya Ukuzaji Mazao Kello Harsama alisema serikali imepanga bei ya kununua ngano kuwa Sh5, 200 kwa gunia ya ngano gredi ya kwanza na Sh5,100 kwa ya pili. Akizungumza wakati wa hafla wa wanahabari ya uzinduzi wa Mkutano wa Afrika wa Teknolojia ya Kilimo (ACAT), katibu alisema chini ya mpango ambao ulikubaliwa kati ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo, Chama cha Wasagaji nafaka na wakulima wa ngano, Chama cha Wasagaji nafaka kinatakiwa kununua ngano yote nchini kabla ya kuruhusiwa kuagiza kutoka nje.

“Chini ya mpango huu, ushuru wa bidhaa kutoka nje ume-punguzwa kutoka asilimia 35 hadi 10 na wasagaji wa ndani wamekubali kwamba kwanza watanunua mavuno yote ndani na hivyo kutoa soko zuri kwa wakulima,” Harsama alisema. Alifafanua kuwa baada ya wasagaji hao kumaliza ngano ya ndani, wataruhusiwa

kuagiza magunia engine milioni mbili kutoka nchi nyingine ili kukidhi mahitaji ya ndani ya takriban magunia milioni tatu kwa mwaka.

“Yanayoendelea kati ya Urusi na Ukraine ambapo usafirishaji wa ngano kutoka Ukraine umesimamishwa yanatia wasiwasi kwa sababu tulikuwa tukipata karibu ngano kutoka Ukraine na wale wanaoagiza ngano wanapaswa kuhakikisha kwamba wanapata usambazaji endelevu wa ngano kutoka vyanzo mbadala,” Katibu alieleza. Harsama aliongeza kuwa pia wanatarajia mavuno mazuri ya mahindi ya takriban magunia milioni 44, ambayo yanatosha kulisha nchi.

“Pia tumeanza kupokea mahindi kutoka Tanzania na Uganda huku tukisubiri mahindi yetu kukomaa. Kutokana na usambazaji wa mahindi kutoka nchi jirani bei ya gunia la mahindi imepungua kutoka Sh6, 000 hadi Sh5, 000,” alisema. Harsama alisema kutokana na kupungua kwa bei ya mahindi, baadhi ya wasagaji wamepunguza bei ya unga kutoka Sh220 hadi Sh175. Na Joseph Ng'ang'a (KNA)

Benki ya Dunia yatenga Sh 105m kusimamia rasilimali za maji Nile

NA CHRIS MAHANDARA (KNA)

Benki ya Dunia imetenga Sh105 milioni kwa utekelezaji wa Mradi wa Ushirikiano wa Pamoja wa Usaidizi kwa Ustahimilivu wa Tabia nchi katika ukanda wa Nile. Utekelezaji huo utafanyika katika nchi zote saba wanachama wa Afrika Mashariki ambazo ni Kenya, Burundi, Rwanda, Tanzania, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na Sudan Kusini. Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Bonde la Ziwa Victoria Mhandisi Colletta Ruhama alithibitisha kuwa benki hiyo tayari

imejitolea kuunga mkono mpango huo ambao lengo lake ni kuboresha mifumo ya ushirikiano katika usimamizi na maendeleo ya rasilimali za maji katika Bonde la Mto Nile.

Mhandisi Ruhama alisema kupitia ufadhili huo, tume itatekeleza ubora wa maji katika bonde dogo la Ziwa Victoria na kuwianisha sera na kuandaa mkakati na mpango kazi.

Alisema, “Tunashukuru msaada mkubwa wa Benki ya Dunia unaojiri wakati idadi kubwa ya watu wanaoishi ndani ya Bonde la Mto Nile wanakabiliwa na

matatizo makubwa. Ufadhili huu utasaidia sana kutatua changamoto zilizopo.”

Ruhama alisema shughuli hizo zitafanyika katika nchi zote saba za Maziwa ya Ikweta ya Nile na nchi wanachama wa Afrika Mashariki. Alisema lengo la jumla la shughuli hiyo litakuwa kuwianisha na kuimarisha sera za ubora wa maji katika nchi za mabonde hayo. Aidha, Mhandisi Ruhama alisema tume hiyo inajadiliana na Benki ya Dunia kuhusu masuala ya bahari na uwezo wa kutambua ubora wa maji na ufuatiliaji wa kiwango cha maji ya Ziwa. “Makatibu ku-

toka nchi saba wanachama wamejitolea kuhakikisha kwamba wanakusanya rasilimali ambazo zitasaidia katika utekelezaji mzuri wa miradi hii,” alisema. Bonde la Mto Nile limekuwa likikabiliwa na vitisho vikubwa miongoni mwao vikiwemo ukataji miti, malisho ya mifugo kupita kiasi, na mmomonyoko wa udongo kutokana na kanuni duni za kilimo ndani ya vyanzo vya ziwa.

Uendelevu wa upatikanaji wa maji pia umebainishwa kuwa changamoto kubwa inayoathiri watu wanaoishi ndani ya bonde hilo.